



HAKUNA UVUTAJI KATI YA BENDERA KWENYE UFUKWE UNAOTEMBELEWA

Sheria Mpya inayozuia uvutaji kuanzia tarehe 22 Septemba 2010

Uvutaji umepigwa marufuku kwenye maeneo yote ya ufukweni yanayotembelewa hapa Western Australia.

Mtu haruhusiwi kuvuta ndani ya eneo lililopo kati ya milingoti yenye bendera au alama zozote zilizoweka kwenye ufukwe kuonyesha kuwa ni eneo linalotembelewa na waogeleaji.

Ufukwe wa bahari unaotembelewa mara nyingi huonyeshwa na:

- Uwepo wa Waokoa maisha
- Bendera mbili za rangi nyekundu na manjano zinazowekwa kwenye mchanga ufukweni
- Bendera zinaashiria kuwa ni salama kuogelea katika eneo linalokingwa.

Tahadhari ya kutokuvuta inafanya kazi pale kipindi bendera hizo zitakuwapo.

Alama

Halmashauri za maeneo husika zinaweza kuweka alama kwenye ufukwe zinazotembelewa ili kuonyesha imepigwa marufuku kuvuta ndani ya eneo hilo.

Hatua za Kisheria

- Serikali ya Mtaa inawajibu wa msingi kutekeleza hatua za kisheria zinazohusiana na kupigwa marufuku uvutaji ufukweni.
- Sheria mpya inaruhusu Halmashauri za maeneo kuchagua maofisa wa Afya au maofisa wa ziada, kwa mfano Rangers, ili kusaidia utekelezaji wake.
- Waokoa maisha waliojitolea hawana jukumu la kutekeleza sheria hizo.

Ni muhimu kuisisitiza kuwa sheria hii mpya inakubalika miongoni mwa jamii kwa kiwango kikubwa sana hivyo basi kutokana uzoefu wetu kutoka kwenye kipindi cha nyuma tunategemea kuwa wanajamii wa Western Australia watafuata na kutekeleza.

Adhabu

Kama kosa la uvutaji limefanyika ndani ya eneo liliowekwa bendera basi adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa kwa mtu aliyefanya kosa hilo:

- Mahakama inaweza kukupa amri ya kulipa kiwango kisichozidi \$1000
- Unaweza kupewa Notisi ya Kulipa \$200

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Tawi linalofuatilia Tumbaku:

Simu: 1300 784 892

Barua pepe/Email: tcb@health.wa.gov.au

Disclaimer:

The information contained in this factsheet has been produced as a guide only. To view the full details in the relevant Tobacco Control legislation, visit www.health.wa.gov.au/tobaccocontrol